

## Kwa nini mtoto wangu atahitaji kipimo kingine cha uwezo wa kusikia katika utotoni?

Sio matatizo yote ya kusikia ya utotoni hutambuliwa wakati wa kuzaliwa. Upotezaji wa uwezo wa kusikia unaweza kutokea wakati wowote kwa sababu nyingi.

Baadhi ya sababu za kuchunguza uwezo wa kusikia wa mtoto wako:

- historia ya familia ya upotezaji wa kudumu wa uwezo wa kusikia utotoni
- kasoro zinazoonekana za kichwa, uso, shingo au masikio
- kama ametumia dawa fulani zinazotolewa wakati wa kuzaliwa kwa zaidi ya siku 5
- utambuzi wa ugonjwa unaojumuisha uwezekano wa upotezaji wa uwezo wa kusikia
- kulazwa katika kitengo cha wagonjwa mahututi cha watoto waliozaliwa papo (NICU) kwa zaidi ya siku 5
- wasiwasi wa familia au mtunzaji
- kuchelewa katika kukuza ujuzi wa usemi na/au lugha

VTEHDI itakutumia barua wewe na mtunzaji wa mtoto wako ikiwa upimaji wa mara kwa mara unapendekezwa.

Kwa taarifa zaidi kuhusu orodha iliyo hapo juu, na saa na mahali pa kupata miadi ya uchunguzi wa uwezo wa kusikia, tembelea **healthvermont.gov/hearing.**

## Mpango wa Msaada na Utambuzi wa Mapema wa (VTEHDI) Uwezo wa Kusikia wa Vermont

Mpango wa VTEHDI hufuatilia matokeo ya uchunguzi wa uwezo wa kusikia kwa watoto wote waliozaliwa katika Vermont ili kuhakikisha watoto wote wanapata uchunguzi na ufuatiliaji wa uwezo wa kusikia kama inavyohitajika na kwa wakati.

Kwa taarifa zaidi, tembelea
**healthvermont.gov/hearing**

Brosha hii:

- imetafsiriwa na inapatikana katika tovuti yetu kwa Kifaransa, Kiarabu, Kiswahili, Kiburma, Kirundi, Kinepali, Kisomali, Kihispania
- ilisasishwa na kubuniwa kwa pamoja na wanafamilia (2022)

VERMONT
DEPARTMENT OF HEALTH

Ugunduzi wa Usikivu wa Mapema wa Vermont na Kitengo cha Afya ya Mama na Mtoto
1-800-537-0076 au 1-802-651-1872
VTEHDI@vermont.gov

# Usikivu wa Mtoto mchanga Uchunguzi



TAARIFA KWA FAMILIA

Mpango wa Msaada na Utambuzi wa Mapema wa Uwezo wa Kusikia wa Vermont

Swahili

## Kwa nini watoto WOTE wanaozaliwa wanapaswa kufanyiwa uchunguzi wa uwezo wa kusikia wanapozaliwa?

- Ni vigumu kubainisha uwezo wa kusikia. Familia hufikiri zinaweza kujua ikiwa mtoto wao hawezi kusikia lakini sivyo wakati mwingine.
- Mtoto 1 hadi 3 kati ya watoto elfu moja huzaliwa na kiwango fulani cha matatizo ya uwezo wa kusikia.
- Uchunguzi wa uwezo wa kusikia kwa watoto walioazaliwa unaweza kugundua upotezaji unaowezekana wa uwezo wa kusikia katika siku za kwanza za maisha.
- Mwaka wa kwanza wa maisha ni muhimu kwa maendeleo ya usemi na lugha. Wakati mtoto hawezi kusikia sauti, anaweza kuwa na ucheleweshaji wa ujuzi huu.
- Ni nusu tu ya watoto walio na matatizo ya kusikia wana historia inayojulikana ya familia ya matatizo ya kusikia au sababu zingine hatari.

## Uchunguzi wa uwezo wa kusikia wa mtoto wangu utafanywa lini?

Uchunguzi wa uwezo wa kusikia unapaswa kufanywa kabla ya kuondoka hospitalini. Hospitali nyingi huchunguza uwezo wa kusikia wa mtoto kati ya saa 12 hadi 24 baada ya kuzaliwa.

Ukiwa utajifungulia nyumbani, mkunga wako atamchunguza mtoto wako ndani ya wiki za kwanza baada ya kuzaliwa.



## Nani atamchunguza mtoto wangu uwezo wa kusikia?

Uchunguzi wa uwezo wa kusikia unaweza kufanywa na mtaalamu wa kusikia, muuguzi, fundi aliyefunzwa, mtaalamu wa mfumo wa kupumua, au mkunga.

## Je, uwezo wa kusikia kwa mtoto wangu utachunguzwaje?

Chunguzi za uwezo wa kusikia ni salama, za haraka, na sio chungu. Watoto wengi huwa wamelala muda wote kwani hakuna jibu linalohitajika kutoka kwa mtoto wako.

Kifaa kidogo huwekwa kwenye upande wa juu au ndani ya masikio ya mtoto wako na sauti laini inachezwa. Kifaa hiki hupima jinsi mtoto anavyojibu, na matokeo yatapatikana wakati uchunguzi unapokamilika.

## Je, ni matokeo gani yanayowezekana ya uchunguzi wa uwezo wa kusikia kwa mtoto mchanga?

**AMEFAULU** inamaanisha hakuna hatua ya ziada inayohitajika kwa wakati huu.

**RUFAA** inamaanisha mtoto hakufaulu uchunguzi wa uwezo wa kusikia. Hii haimanishi kwamba kuna upotezaji wa uwezo wa kusikia, bali kwamba upimaji zaidi unahitajika.

**Haukukamika/Ulijaribiwa** inamaanisha uchunguzi ulipaswa kusimamishwa mapema na uchunguzi mwingine unahitajika. Hii inaweza kuwa ni kutokana na kiwango cha shughuli za mtoto, kelele katika mazingira au matatizo na kifaa.

Matokeo ya uchunguzi wa uwezo wa kusikia wa mtoto wako yatashirikiwa nawe, mtoa huduma wa afya ya mtoto wako na Mpango wa VTEHDI.

## Itakuwaje ikiwa mtoto wangu hakufanyiwa uchunguzi wa uwezo wa kusikia au anahitaji uchunguzi mwingine?

Mpango wa VTEHDI utakupigia simu wewe na/au daktari wa mtoto wako ili kusaidia kufanya miadi isiyo ya kulazwa. Unaweza pia kuwasiliana na VTEHDI (angalia maelezo ya mawasiliano nyuma ya brosha hii).

Unaweza kwenda kwa miadi isiyo ya kulazwa katika hospitali ya jamii, ofisi ya wataalamu wa kusikia au ofisi ya mtoa huduma ya afya ya watoto.



### Tunatumia mbinu* ya 1-3-6

**1** - Kuchunguza watoto wote waliozaliwa kabla ya kuondoka hospitalini au kabla ya **1kufikisha mwezi**wa umri.

**3** - wanaohitaji uchunguzi zaidi wanapimwa kabla ya kufikisha **miezi 3ya** umri.

**6** - wanaopatikana na kiwango fulani cha matatizo ya kusikia watapendekezewa na kuandikishwa katika huduma za msaada wa mapema kabla ya kufikisha **miezi 6ya** umri.

* *Kulingana na Miongozo ya Tume ya Pamoja ya Kitaifa ya Uwezo wa Kusikia wa Watoto Wachanga (JCIH).*

Swahili